

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990  
Telegramu: Railways  
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu  
S.L.P 70364  
Dar es Salaam  
26 Oktoba 2019

---

## TAARIFA KWA UMMA

### **KUSITISHWA KWA HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI KATIKA UKANDA WA KASKAZINI HUSUSANI TANGA NA MKOA WA KILIMANJARO KUENZIA TAREHE 26.10.2019.**

Shirika la Reli Tanzania linaomba radhi kwa wateja wake kutokana na kusitishwa huduma zinazotolewa na TRC hasa usafirishaji wa mizigo katika ukanda wa kaskazini yaani Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga kuanzia tarehe 26.10.2019.

Shirika la reli Tanzania limesitisha utoaji wa huduma kutokana na mvua kubwa za vuli zinazoendelea kunyesha katika ukanda wa kaskazini na kusababisha mito ya pangani (Ruvu ) na Rwengera kuacha njia yake baada ya kujaa maji na kuelekea relini.

Tukio hilo limesababisha uharibifu wa miundombinu ya reli yakiwemo madaraja, sehemu zilizoathirika ni : Muheza, Korogwe hadi Mombo sehemu kubwa ya reli imeathirika na yakiwemo madaraja mawili. Eneo lingine lililoathirika ni Wami- Makinyumbi (Hale) na kufanya uharibifu wa makaravati manne.

Shirika linaendelea kuomba radhi kwa wateja kutokana na usumbufu uliojitokeza na tutaendelea kuwahabarisha pale njia itakapotengemaa na kuendelea na utoaji wa huduma kama ilivyo awali. Kwa uhitaji wa taarifa sahihi kuhusu TRC, unaweza fungua tovuti ya TRC na kupata taarifa za uhakika [www.trc.co.tz](http://www.trc.co.tz) au fungua mitandao ya kijamii “Facebook, Twitter, instagram kwa anuani tzrailways au kutumia simu ya huduma kwa wateja ya bure ambayo ni : 0800110042.

---

Imeandaliwa na Ofisi ya Uhusiano kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu  
Shirika la Reli Tanzania